

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**SALAAMU KUTOKA KWA MRATIBU WA MKURABITA
KATIKA HAFLA YA UZINDUZI WA UTOAJI HATI MILIKI
KWA WAKAZI WA IDUNDILANGA, HALMASHAURI YA MJI
WA NJOMBE, 19 JUNI 2010**

- Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mkuu wa Mkoa Iringa Mohamed Abdulaziz (MB)
- Mheshimiwa Naibu Spika na Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi wa MKURABITA, Anna Makinda (MB)
- Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Sara Dumba
- Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Edwin Mwanzinga
- Waheshimiwa Madiwani
- Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe
- Waheshimiwa Wageni Waalikwa
- Mabibi na Mabwana
- Wadau wote wa Urasimishaji
- Itifaki imezingatiwa

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi kutoa salaamu kutoka kwa Mratibu wa MKURABITA, Eng. Ladislaus Salema ambaye ameomba radhi kwa kushindwa kufika hapa kutokana na kuwa katika Kikao cha Bunge cha Bajeti kinachoendelea mjini Dodoma.

Hivyo kwa niaba ya Mratibu wa MKURABITA, napenda kusema kwamba MKURABITA tulikuja hapa Idundilanga kuanza utekelezaji wa baadhi ya mapendekezo ya maboresho ya urasimishaji ardhi mijini.

Vile vile tulikuja kwa nia ya kuthibitisha kuwa wananchi wakihamasishwa na kuelimishwa zaidi juu ya dhana ya uwezesaji, ushiriki wao unakuwa ni mkubwa. Na ushiriki wa wananchi ukiwa mkubwa unafanya gharama za urasimishaji kuwa ndogo na zenye unafuu kwa walengwa.

Kwa hiyo kwa kupitia zoezi la urasimishaji hapa Idundilanga tumejifunza mengi. Kubwa tulilojifunza ni kwamba maelekezo ya Serikali kwa kila Halmashauri kuwa na mfuko wa urasimishaji ni jambo linalowezekana na lenye manufaa kama ambavyo tunashuhudia leo hii hapa mjini Njombe.

Aidha tumetumia nafasi tuliyopata wakati wa urasimishaji hapa Idundilanga, kutoa elimu kwa walengwa juu ya umuhimu wa kurasimisha miliki zao na hatimaye kuzitumia katika kujiletea maendeleo.

Mwisho naomba kuisisitiza kwa wananchi ambao leo hii mmekabidhiwa Hati Miliki, kuhakikisha kuwa mnazitumia kikamilifu kwa kadri fursa zitavyopatikana ili kujiletea maendeleo zaidi kiuchumi kama dhana ya MKURABITA ilivyo; *Uwezesaji wananchi kutumia rasilimali na biashara zao kama chanzo cha kujiongezea mitaji na nyenzo ya kupanua wigo wa ushiriki katika shughuli za uchumi wa kisasa.*

Na kwa wenzetu wa taasisi za fedha, tunawaomba mazitambue na kukubali kutumia hati hizi kama dhamana kwa ajili ya maombi ya wananchi watakaohitaji kupata mikopo ili kuboresha zaidi uzalishaji na shughuli zao zingine za kiuchumi.

Ndugu Mgeni Rasmi, Maboresho ya Kisheria na Kitaasisi yaliyobuniwa na MKURABITA ni hai na endelevu. Tulichojifunza hapa Idundilanga kitatusaidia kuimarisha mapendekezo yetu juu ya mabadiliko mbalimbali ya sheria za ardhi yaliyomo kwenye maboresho tunayoyatekeleza

Nawashukuruni sana naomba kuwasilisha,